

Upitishaji Wa Virusi Vya Ukimwi Kutoka Kwa Mama Hadi Kwa Mwanaye Ambaye Hajazaliwa Na Eleanor Turnbull

Virusi vya ukimwi hupatikana katika damu Na maji maji yoyote ya mwili Kama vile maziwa ambaye mama humnyonyesha mwanaye mchanga. Virusi hivi huumiza CD4 na kuzimaliza nguvu ili siziweza kufanya kazi yao vizuri.

CD4 huongeza kinga mwilini ,virusi vya ukimwi huzimaliza nguvu na kwa hivyo mwili hukosa nguvu ya kujikinga kwa ugonjwa zingine na mtu hushikwa na ugonjwa wa ukimwi ambayo ni ugonjwa wa maisha na hauna dawa.

Virusi hivi hupitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia tofauti kama vile kutoka kwa mama hadi kwa mwanaye na pia kama hatumi madawa asilimia ishirini na tano (25%) hupitisha virusi hivi kwa wanawe.

Njia Za Kupitisha Virusi

Mama Mja mzito anaweza kupitisha virusi vya ukimwi kwa mwanawe wakati ana mimba, wakati wa uchungu ya kuzaa,wakati wa kuzaa na mwishoye wakati ana mnyonyesha. watoto kati ya asilimia kumi na tano hadi thelathini na tano (15% - 35%) huenezewa virusi hivi wakati wa kuzaliwa. Mtoto anaweza kupata virusi vya ukimwi kama mama yake ako na nambari ya juu ya virusi hivi kwenye damu au tayari ako na ugonjwa wa ukimwi ; pia kama ana ugonjwa wowote wa zinaa,ama anatumia madawa ya kulevya na pia kama ali ambukizwa virusi akiwa tayari na mimba.

Nchi zenye wamama wengi waja wazito wenye virusi vya ukimwi kama kenya ,asilimia kumi na sita (16%) na zambia asilimia ishirini na nne(24%) kwa kila watoto kumi wanaozaliwa mmoja ana virusi vya ukimwi. Watoto wanaoambukizwa virusi duniani ni asilimia kumi (10%) na asilimia arubaini (40%) wanaoambukizwa virusi kupitia maziwa ya kunyonya wakiwabado wachanga. Njia za kufundisha watu njia za kuchunga wanao zimeanzishwa Afrika ili kujaribu kuteremsha nambari ya watoto wanao ambukizwa.

Njia za kujikinga kutokana na virusi

Njia mingi za kuzuia ziko lakini utumiaji wa madawa ndio njia rahisi.

Njia ya kwanza ni kuhakikisha wamama na wasichana hawaambukizwi virusi and pia kuwafundisha njia za kupanga uzazi kwa kuwafundisha umuhimu wa kutumia kondomu na pia kuwafundisha njia za kujichunga na wanaume wanao watumia vibaya ; wasichana kutoka fmilia za kimaskini hudanganywa na pesa na wanaume wazee ambao huwapatia pesa ,wanaume hawa wengi wao wana virusi vya ukimwi.

Njia nyingine ni kwamba wamama wote waja wazito wanafaiwa kujua hali ya ukimwi kwani watu wengi ambao wana virusi hivi hawajui hali zao karibu asiimia tisini (90%) ,wengi wao wanaogopa kupimwa kwani jamii na jamaa wao wata wadharau , wata wafukuza na kuwanyang"anya watoto wao na mali zao. pia mam akipatikana na virusi analaumiwa ni yeye alileta kwa familia.

Familia zinapaswa kufundishwa kutodharau hali ya wamama hawa na pia hospitali zinapaswa kuwafundisha wamama njia za kumeza madawa na pia njia za kuishi salama pia zinapaswa kuweka matokea ya mgonjwa siri na ni yeye tu(mama) anaweza kujulisha familia yake wakati anapotaka.

Njia za kuzuia mama kupitisha virusi kwa mtoto ambaye hajazaliwa

Madawa ndio njia muhimu kabisa wa kuzuia uenezaji wa virusi kutoka kwa mama hadi mwanaye ,dawa za muda mfupi kama nevirapine na zidovudine zinapeanwa wakati mama ako karibu kuzaa na wakati anapo zaa pia kama mama ameamua kupasuliwa na hii huteremsha kuambukiza virusi kwa asilimia mbili(2%) au chini. Dawa ambayo imeonyesha matokeo mazuri kabisa inaitwa zidovudine mama anapatiwa mimba ikiwa wiki ishirini na nane na anapatiwa mara mbili kwa siku , pamoja na dawa nyingine inayoitwa nevirapine ambayo hupatiwa mtoto pia anapo zaliwa. Mama anaweza kushindwa kufatanisha maagizo ya madawa haya na kama hii ndio sababu basi mama hupewa dawa ya nevirapine na kushauriwa kuimeza wakati ana sikia uchungu wa kuzaa na mtoto anafaiwa kupewa kabla ya masaa sabini na mbili kutoka azaliwe na hii huteremsha hatari ya mtoto kupatwa na virusi na nusu ama kuteremshwa na asilimia kumi (10%). Njia imefaulu na ni rahisi kwa nchi ambazo hazijiwezi kama vile lusaka ambapo maelfu ya wamama wamepimwa kwa kujitakia na kupewa madawa, wamama ambao humeza madawa wakati wana mimba watoto wao huzaliwa bila shida na hukua vizuri ; kuna ripoti ambazo zinaonyesha wamama wengine hawasaidiwi na madawa haya lakini bado utafiti unafanywa.

Upitishaji Wa Virusi Vya Ukimwi Kupitia Maziwa Ya Mama

Wamama hupata wakati mgumu wanapotaka kuchagua njia ya kulisha wanao ili kuzuia kueneza virusi kwa wanao au magonjwa mengine ambayo hushika watoto ambao hawanyonyeshwi. Kwa nchi zinazoendelea asilimia hamsini na nne (54%) ya watoto ambao hawanyonyeshwi huaga dunia kwani hawapati lisho bora.

Jumuiya ya kimataifa WHO inaeleza ya kwamba maziwa ya mtoto isipokuwa maziwa ya mama inakubaliwa wakati maziwa hiyo ni safi, rahisi ,na inapatikana. Wakati wa kuchagua maziwa ya mtoto lazima maji masafi ya tumike kama hakuna maji masafi basi mtoto anapaswa kunyonyeshwa na mama yake kwa miezi sita bila kupewa kitu kingine chochote. Ripoti zinaonyesha watoto ambao huchanganishiwa vyakula kabla ya kufika miezi sita wana hatari ya kupata virusi hivi na pia kutapika na kuharisha kila wakati.

Mwishowe

Kwa ufupi wamama wote ambao wana ishi na virusi vya ukimwi wana weza kutumia njia ambazo ziko ili kuteremsha hatari ya kueneza virusi hivi kwa wanao ;ingawa njia hizi hazina uhakika asilimia mia moja (100%) na ziko tu kwa wamama kidogo.

Hii ni kwa sababu wamama na wasichana wamewekwa chini na jamaa na hii inawazuia kwenda mahospitali na kupata matibabu na hii inafaiwa kurekebishwa.

Pia kudharauliwa kwa watu walio na virusi hii , inawazuia kwenda hospitali na kupata matibabu na pia hii ina faiwa kurekebishwa na watu wote.

jamaa na familia wana faa kufundishwa na kuelezewa njia ya kuishi na watu walio na virusi hivi na pia njia ya kujichunga ili wasipate virusi hivi.

wamama waja wazito pia wana paswa kufundishwa njia za kuchunga wanao ambao hawajazaliwa kupata virusi vya ukimwi.

REFERENCES// USAIDIZI KUTOKA

Connor EM, Sperling RS, Gelber R, et al. Reduction of maternal-infant transmission of human immunodeficiency virus type 1 with zidovudine treatment. *New England Journal of Medicine* 1994;331:1173–1180

De Cock, K.M., Fowler, M.G., Mercier, E., De Vincenzi, I., Saba, J., Hoff E, et al. Prevention of mother-to-child HIV transmission in resource-poor countries: translating research into policy and practice. *JAMA* 2000, 283:1175–1182

Prevention of mother-to-child transmission of HIV in Africa: successes and challenges in scaling-up a nevirapine-based program in Lusaka, Zambia. *AIDS*. 17(9):1377-1382, June 13, 2003. Stringer, Elizabeth M a-c; Sinkala, Moses a-d; Stringer, Jeffrey SA a-c; Mzyece, Elizabeth c; Makuka, Ida c; Goldenberg, Robert L a,c; Kwape, Pascal e; Chilufya, Martha e; Vermund, Sten H a,c

Fylkesnes K, Musonda R, Kasumba K, Mubanga, Musonda R, Sichone M. The HIV epidemic in Zambia: socio-demographic prevalence patterns and indications of trends among childbearing women. *AIDS* 1997, 11:339–345.

UNAIDS/WHO Policy (2004): www.who.int/bulletin/volumes/84/1/52.pdf

Integrating prevention of mother-to-child HIV transmission into antenatal care: learning from the experiences of women in South Africa. M.-a. Etiebet A1, D. Fransman A2, B. Forsyth A3, N. Coetzee A4, G. Hussey A2

CDC. Revised recommendations for HIV screening of pregnant women. *MMWR* 2001;50(No. RR-19):59–85

AIDS. 17(9):1377-1382, June 13, 2003.

Stringer, Elizabeth M a-c; Sinkala, Moses a-d; Stringer, Jeffrey SA a-c; Mzyece, Elizabeth c; Makuka, Ida c; Goldenberg, Robert L a,c; Kwape, Pascal e; Chilufya, Martha e; Vermund, Sten H a,c

http://www.globaltreatmentaccess.org/content/tx_prep/mtct.html

Mother to Baby Transmission fact sheet -- AIDSMap at:

<http://www.aidsmap.com/publications/factsheets/fs28.htm>

HIV and Infant Feeding, WHO, 2003

WHO Guidelines